


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
BUNGE LA TANZANIA**



MKUTANO WA KWANZA

YATOKANAYO NA KIKAO CHA NNE

20 NOVEMBA, 2015

MKUTANO WA KWANZA
YATOKANAYO NA KIKAO CHA NNE - TAREHE 20 NOVEMBA, 2015

I. DUA:

Saa 3.00 asubuhi Mheshimiwa Job Y. Ndugai (Spika) alisoma Dua na kuongoza Kikao cha Bunge.

Kikao kilianza saa 9:00 Alasiri kikiongozwa na Naibu Spika

Makatibu Mezani:

1. Nenelwa Mwihambi
2. Charles Mloka
3. Asia Minja

II. KIAPO CHA UAMINIFU:

Mhe. Suleiman Masoud Nchambi aliapa kiapo cha Uaminifu.

III. TAARIFA YA SPIKA:

Kiti kilitoa Taarifa ya Mheshimiwa Rais kulihutubia Bunge saa 10:00 jioni

MATANGAZO:

- Wabunge walishauliwa kujaza fomu za Maadili na kuzirejesha mapema
- Wabunge walitaarifiwa kurudisha fomu za maelezo Binafsi na za Kamati

IV. KUTENGUA KANUNI:

Kanuni ya 139(1) na 143 (f) ilitenguliwa ili kuruhusu wageni wasioruhusiwa kungia Bungeni kuruhusiwa kuingia na kukaa

MWONGOZO WA SPIKA:

Mheshimiwa Tundu Lissu aliomba mwogozo na kuhoji kama uamuzi wa kuwakaribisha Rais wa Zanzibar, Makamu wa Rais na Spika wa Baraza la Wawakilishi ni sawa Kikanuni au siyo sawa.

Kiti kilitoa Mwongozo kuwa Ibara 26(1) ya Katiba inaruhusu Viongozi hao waingie Ukumbini.

V. KUSITISHA BUNGE:

Saa 9:10 Bunge lilisitishwa hadi saa 9.30 alasiri.

VI. BUNGE KUREJEA:

Saa 9:30 alasiri Bunge lilirejea kwa Viongozi wafuatao wa Kitaifa kuingia ndani ya Ukumbi wa Bunge:-

1. Jaji Mkuu wa Zanzibar;
2. Jaji Mkuu wa Jamhuri ya Muungano;
3. Spika wa Baraza la wawakilishi Zanzibar;
4. Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar;
5. Rais wa Zanzibar;
6. Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano akiongozwa na Naibu Spika.

Baadaye uliingia msafara wa Spika wa Bunge na Raisi wa Jamhuri ya Muungano Mhe. John Joseph Pombe Magufuli.

Baada ya hapo upande wa Upinzani ulipaza sauti za kuimba na kuomba miongozo kwa fujo, Mheshimiwa Spika aliwataka watoke nje ya Ukumbi wa Bunge na Wabunge wote wa Upinzani walitoka Ukumbini.

VII. UFUNGUZI RASMI WA BUNGE JIPYA:

Mhe. Rais alitoa Hotuba yake na ufunguzi Rasmi Bunge la Kumi na Moja.

Baada ya Hotuba ya Rais kutolewa Mheshimiwa Spika alitoa neno la shukrani na kuwatammbulisha viongozi wa kitaifa na wageni mbalimbali waliohudhuria Shughuli za ufunguzi wa Bunge jipy.

VIII. HOJA YA KUAHIRISHA BUNGE:

Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa (Waziri Mkuu) alitoa Hoja ya kuahirisha Bunge hadi tarehe 26 Januari, 2016. Hoja iliungwa mkono na wabunge kwa kuafiki baada ya kuhojiwa.

IX. WIMBO WA TAIFA:

Wimbo wa Taifa uliimbwa kisha Mheshimiwa Spika aliliahirisha Bunge hadi siku ya Jumanne tarehe 26 Januari, 2016.

**DODOMA
20 NOVEMBA, 2015**

**DKT. T. D. KASHILILAH
KATIBU WA BUNGE**